



>>> Orientation to Ontario

ELIMU YA BAADA YA SHULE YA UPILI

VYUO ANUAI NA VYUO VIKUU

Vyuo vikuu vinatoa mipango inayozingatia taaluma inayoongoza kwa kazi katika teknolojia, afya, biashara, hoteli, utalii na kazi zingine. Mipango ya cheti kawaida huhitaji mwaka mmoja wa masomo. Mipango ya Diploma inahitaji miaka miwili au mitatu ya masomo ya wakati wote. Kwa habari zaidi kuhusu vyuo vya Ontario, tembelea ontariocolleges.ca.

Vyuo vikuu vinatoa mipango ya kitaaluma ya shahada ya kwanza (bachelor) na walio na shahada ya kwanza (uzamili na Uzamifu) katika sanaa na sayansi, na vile vile mipango ya kitaalam katika elimu, udaktari, daktari wa meno, uanasheria na uhandisi.

Kwa habari zaidi kuhusu vyuo vikuu vya Ontario, tembelea Kituo cha kutuma Maombi cha Vyuo Vikuu vya Ontario kwa ouac.on.ca

KUANDIKISHWA CHUONI

Kwa ujumla, diploma ya shule ya upili au sekondari inahitajika ili kuandikishwa kwa chuo anuai au chuo kikuu. Ikiwa hukuhitimu kutoka shule ya upili, unaweza kutuma ombi kama mwanafunzi mkomavu kulingana na uzoefu wako. Wanafunzi waliokomaa lazima wawe na umri wa miaka 19 au zaidi na raia wa Kanada au mkazi wa kudumu.

Ili kujifunza kuhusu tarehe muhimu za kuandikishwa katika vyuo vikuu, tembelea Kituo cha kutuma Maombi cha Vyuo Vikuu vya Ontario

kwa ouinfo.ca

Bodi nyingi za shule huko Ontario hutoa mipango ya diploma ya shule ya upili bila malipo kwa watu wazima. Tembelea tovuti ya bodi ya shule iliyo karibu nawe kwa maelezo zaidi.

Pia inawezekana kukamilisha diploma yako ya shule ya upili mtandaoni. Tembelea Kituo cha Kujitegemea cha Kujifunza kwenye ilc.org

Unaweza kupata mkopo kwa kozi ulizomaliza katika chuo kikuu cha ng'ambo au chuo anuai. Kila taasisi ina mchakato wake wa tathmini.

Kwa habari zaidi kuhusu vyuo anuai na vyuo vikuu vya Ontario, tembelea Wizara ya Mafunzo, Vyuo Anuai na Vyuo Vikuu: ontario.ca au findlink.at/findschool

Kwa taarifa kuhusu vyuo anuai na vyuo vikuu vinavyotumia lugha ya Kifaransa, tembelea Wizara ya Mafunzo, Vyuo Anuai na Vyuo Vikuu katika ontario.ca au findlink.at/Frenschool

MSAADAA WA KIFEDHA

Wanafunzi katika vyuo anuai na vyuo vikuu vya Ontario wanaweza kustahiki msaada wa kifedha kutoka kwa Mpango wa Usaidizi wa Wanafunzi wa Ontario (OSAP). Kwa habari zaidi, tembelea osap.gov.on.ca

Serikali ya jimbo pia hutoa pesa kuititia mpango wa Mikopo ya Wanafunzi wa Kanada: canada.ca

Funded by / Financé par :

MAFUNZO YA USOMI

Mwanafunzi anajifunza ufundi wa stadi kazini, chini ya uongozi wa wafanyakazi wenye usoefu. Kama mwanafunzi, unachukuliwa kuwa mfanyakazi na unapata mshahara. Zaidi ya ufundi 150 unaweza kujifunza kuititia mafunzo ya usomi.

Jifunze zaidi kuhusu mafunzo ya usomi kwenye ontario.ca au findlink.at/trades

Jifunze kuhusu Mpango wa Mafunzo ya usomi wa Vijana wa Ontario kwa wanafunzi wa shule ya upili katika oyap.com



JE, UNAJUA?

Vyuo vya taaluma ya kibinafsi huko Ontario havidhibitiwi kwa njia sawa na vyuo vya umma, na vinatoza ada ya juu.

Ni muhimu kutafiti chaguzi zote kwa uangalifu.

